

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



### MWALIKO KWA WADAU WA KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KAMATI YA SERA ZA KODI (TASK FORCE ON TAX REFORM) KWA AJILI YA MATAYARISHO YA BAJETI YA 2010/11

Kamati ya Ushauri wa Sera za Kodi (Task Force on Tax Reform) kwa ajili ya matayarisho ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2010/11 itaanza kazi yake mwezi Februari, 2010. Sekretariati ya Kamati inaandaa mkutano wa Wadau, kwa ajili ya kuwasilisha mada na kuzijadili. Serikali itaongoza mjadala kwa kutoa malengo yake ya sera, agenda, changamoto na kutathmini vipaumbele vya sera za mapato katika bajeti ya 2010/11. Hali hii itawapa washiriki mtazamo mpana zaidi kuhusiana na shughuli za mwaka huu na kuhamasisha uchambuzi na majadiliano ya mapendekezo mbalimbali kwa undani zaidi.

Sera za mapato zinalenga kupanua wigo wa kodi, kuboresha zaidi mfumo wa kodi na taratibu za ukusanyaji, kuongeza ufanisi wa ukusanyaji na udhibiti wa ukwepaji wa kodi. Aidha lengo kuu la Serikali ni kuweka mfumo wa kodi wenye kuboresha mazingira ya uwekezaji na uzalishaji ili kukuza uchumi.

Kamati inakaribisha ushiriki wa Maafisa wa Serikali, sekta binafsi, Asasi zisizo za Kiserikali, taasisi za dini, jamii ya wasomi, taasisi za utafiti, na wataalam wengine katika sekta mbalimbali za uchumi wa umma.

Aidha, Kamati inakaribisha mada mbalimbali kimaandishi kutoka kwa wale wanaopenda kufanya hivyo. Mada hizo hazina budi kuonyesha yafuatayo:-

- Mtu, kampuni/makampuni, taasisi au chama/vyama ambavyo wanawakilisha;
- Mapendekezo ya mabadiliko katika mapato ya Serikali yanayotokana na kodi na yasiyotokana na kodi, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa sekta, mikoa au aina ya walipa kodi ambao wataathirika, na kwa njia ipi;
- Makisio ya athari kwenye uchumi na kwa mapato ya Serikali katika mwaka huu wa utekelezaji na pia katika miaka ijayo;
- Sababu na uhalali wa mapendekezo ya mabadiliko kwenye sera za mapato na hususan uchambuzi wa namna ambavyo mapendekezo hayo yataisaidia serikali kufanikisha malengo yake makuu ya kiuchumi, kodi na kupunguza umasikini.
- Pale ambapo mapendekezo yanapunguza mapato ya Serikali (hata katika kipindi cha muda mfupi), mapendekezo hayo hayana budi yaweke bayana hatua za kuaminika sambamba na msukumo wa jumla wa sera za bajeti ya serikali ili kufidia upungufu wa mapato ambao utajitokeza/unatarajiwa.

Kamati ya ushauri wa Sera za Kodi kwa muda mrefu sasa imekuwa ikifanikisha mikutano kwa ajili ya majadiliano ya masuala mbalimbali yanayohusiana na sera za kodi na usimamizi wake. Mikutano hii imekuwa ikitoa mchango mkubwa kwa waandaa sera (policy makers) kwa zaidi ya miaka kumi na mbili iliyopita. Hali hii imesaidia sana kuunda mfumo wa kodi nchini ambao kwa kupitia majadiliano/mazungumzo na uchambuzi umewezesha utatuzi wa masuala mbalimbali ya kodi kwa ufasaha wa uwazi. Tunategemea tena kuendelea na majadiliano haya kati ya wadau katika masuala mbalimbali ya Uchumi.

Mwisho, Mada zote na maoni ziwasilishwe kuanzia sasa hadi tarehe 20 Februari, 2010 kwenye Sekretariati ya "Task Force on Tax Reform", Wizara ya Fedha na Uchumi, Idara ya Sera, Chumba Na. 339 (Jengo Kuu la Hazina), Dar Es Salaam.

Ramadhani M. Khijjah  
KATIBU MKUU – FEDHA NA UCHUMI

Januari, 2010

